JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2022

## KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2022

# 021 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

YALIYOMO .......... iii

DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI .......... 2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA .......... 2

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua .......... 2

2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha .......... 13

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI .......... 16

2.2.1 Swali la 3: Ufahamu .......... 16

2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno .......... 21

2.2.3 Swali la 5: Aina za Maneno .......... 25

2.2.4 Swali la 6: Dhima ya Lugha .......... 28

2.2.5 Swali la 7: Sifa za Misimu .......... 31

2.2.6 Swali la 8: Fasihi Simulizi .......... 34

2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi .......... 39

2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU (INSHA) .......... 42

2.3.1 Swali la 10: Uandishi wa Insha .......... 42

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA .......... 46

4.0 HITIMISHO .......... 47

5.0 MAPENDEKEZO .......... 48

KIAMBATISHO A: UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2022 .......... 49

KIAMBATISHO B: ULINGANIFU WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2021 NA 2022 .......... 50

# DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili mwaka 2022 imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu kuhusu matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya kati inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Kimsingi uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu unalenga kuonesha dhahiri yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha Sekondari, Kidato cha Kwanza na cha Pili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za wanafunzi kufanya vizuri, vibaya au au kwa kiwango cha wastani katika maswali/mada mbalimbali zilizopimwa. Ripoti hii inaonesha baadhi ya sababu zilizofanya wanafunzi kufanya vizuri kama vile kuwa na uelewa mzuri wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya swali. Pia sababu za wanafunzi kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zimeelezwa kuwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheza. Aidha, sababu zilizofanya wanafunzi wachache kupata alama hafifu katika majibu yao zimefafanuliwa kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kuelezea dhana mbalimbali kwa ufasaha, na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa jumla.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Pia Baraza linaamini kuwa, mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yakizingatiwa ipasavyo, kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka katika upimaji ujao.

Mwisho, Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha Pili uliofanyika mwezi Novemba mwaka 2022 ulikuwa na maswali kumi (10). Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu A, B na C ambapo sehemu A ilihusu maswali ya kuchagua na kuonisha; sehemu B maswali ya majibu mafupi na sehemu C ilikuwa na swali la insha. Mada zilizotahiniwa katika sehemu zote zilihusisha *Ufahamu*, *Sarufi*, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*, *Fasihi* na *Uandishi/Utungaji*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu umezingatia kikamilifu muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha Kwanza na cha Pili.

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Pili katika Upimaji wa somo la Kiswahili mwaka 2022. Jumla ya wanafunzi 690,337 walisajiliwa kufanya upimaji ambapo wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 91.96 walifanya upimaji wa somo la Kiswahili. Miongoni mwao, wavulana walikuwa 292,709 (46.11%) na wasichana 342,134 (53.89%). Ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu kwa ujumla ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 605,767 sawa na asilimia 95.66 ya wote waliopimwa walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha ufaulu ni cha juu kwa asilimia 0.45 kikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo, asilimia 95.21 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Ulinganifu wa ufaulu wa wanafunzi kwa kila daraja kwa mwaka 2021 na 2022 umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Wanafunzi kwa Kila Daraja**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Madaraja** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2021 | 601,458 | 52,339 | 114,525 | 302,851 | 103,220 | 28,842 |
| 2022 | 634,843 | 78,986 | 107,914 | 289,808 | 129,059 | 27,486 |

**Jedwali Na**. **1** linaonesha kuwa viwango vya ufaulu vimeongezeka na kupungua kwa baadhi ya madaraja kwa mwaka 2022. Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa daraja A na D ndiyo yaliyoongezeka ufaulu na idadi ya wanafuzi waliopata daraja F imepungua ikilinganishwa na mwaka 2021.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni kiwango *kizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100, kiwango cha wastani kikianzia alama 30 hadi 64, na kiwango hafifu ni kuanzia alama 0 hadi 29. Chati mbalimbali zimetumika kufafanua viwango hivyo. Aidha, rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kiwango cha wastani na rangi nyekundu inawakilisha kiwango hafifu cha ufaulu. Vilevile, sampuli za majibu sahihi na yale yasiyo sahihi kutoka kwa wanafunzi zimeambatanishwa ili kudhihirisha majibu halisi ya wanafunzi.

Kwa jumla, uchambuzi huu unalenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili.

# 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inaonesha uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyojibiwa vizuri na yale yaliyojibiwa vibaya. Aidha, sababu za ufaulu wa viwango mbalimbali zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya wanafunzi kwa kila swali zimeambatanishwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa katika uchambuzi huu.

## 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua lenye vipengele kumi (10) na swali la 2 lilikuwa la kuoanisha maelezo na dhana katika orodha A na B. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali lilitoka katika mada za *Fasihi Simulizi, Matumizi ya Lugha, Aina za Maneno, Usimulizi, Uandishi na Uundaji wa Maneno*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka dhana mbalimbali zinazohusu mada anuwai za somo la Kiswahili. Swali lilimtaka mwanafunzi kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo manne (A – D) kwa kila kipengele.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji katika somo hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi ambapo asilimia 88.91 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 1***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1.*

Chati Na. 1 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo wanafunzi 188,739 (29.73) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 9, wanafunzi 375,703 (59.18%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 5.5 na wengine 70,401 (11.09%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa asilimia 59.18 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana mbalimbali zilizopimwa katika baadhi ya vipengele vya swali hili. Wanafunzi hao waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 3 – 5 na kupata alama za wastani.

Wanafunzi wengine 188,739 sawa na asilimia 20.73 walijibu vizuri swali hili kwa kuonesha umahiri wa dhana zilizopimwa katika mada husika. Kwa ujumla wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele vingi vya swali hili kwa kuchagua herufi yenye jibu

sahihi. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele (i - x) na kupata alama zote.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Seti ipi ni sahihi kuhusu vipengele vya fani katika fasihi simulizi?
A Dhamira, migogoro, mtindo na mafunzo.
B Ujumbe, matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na muundo.
C Wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari.
D Migogoro, ujumbe, wahusika, mafunzo na mtindo.

[ C ]

(ii) Ni muundo upi wa ushairi wa fasihi simulizi unaundwa na mistari/mishororo mitano?
A Sabilia B Takhmisa
C Tathmisa D Tathilitha

[ B ]

(iii) Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yana athari chanya na hasi katika ukuaji wa fasihi simulizi. Zipi ni athari hasi zinazoikabili fasihi simulizi?
A Hupunguza hadhi na ubora wa kazi za fasihi.
B Huhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa muda mrefu.
C Huboresha uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi.
D Hutunza kiini au maana ya ujumbe wa fasihi simulizi.

[ A ]

(iv) Sababu zifuatazo husababisha kutokea kwa utata katika tungo, **isipokuwa**:
A Neno kuwa na maana zaidi ya moja.
B Kuzingatia taratibu za uandishi.
C Kutumia maneno yenye maana ya picha.
D Kutotamka neno ulilokusudia kwa usahihi.

[ B ]

(v) Juma huimba vizuri <u>sana</u>. Neno linalopigiwa msitari linafanya kazi ya aina ipi ya neno?
A Kielezi B Kivumishi
C Kitenzi D Kihisishi

[ A ]

(vi) Wewe na rafiki yako mmepewa kazi ya kubainisha sentensi yenye vivumishi vya ***a-unganifu*** katika tungo. Je, ni sentensi ipi kati ya zifuatazo itakuwa sahihi?
A Juma anacheza kwa madoido.
B Halima mrefu amefika.
C Abdul na Zuberi wameondoka jana.
D Janeth wa Dodoma ameingia darasani.

[ D ]

(vii) Kati ya kanuni zifuatazo mojawapo **si** sahihi kuhusu usimulizi wa matukio.
A Kutamka matamshi kwa usahihi.
B Mpangilio mzuri wa mawazo.
C Kujua muundo wa matukio.
D Kutumia lugha kwa usahihi.

C

(ix) Ipi ni dhima sahihi ya kutumia picha na michoro katika kamusi?
A Hufanya kamusi kutambulika kwa haraka.
B Hufanya kamusi kupendwa na wasomaji.
C Hupunguza umakini na idadi ya watumiaji.
D Husaidia wasomaji kuwa na kumbukumbu.

D

(x) Ipi ni maana sahihi ya shina la neno kati ya zifuatazo?
A Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali na tamati.
B Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali pekee.
C Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati pekee.
D Sehemu ya neno yenye mzizi na kiambishi tamati vijenzi.

C

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na.1.1, mwanafunzi aliweza kuchagua herufi za majibu sahihi kutokana na kuwa na uelewa wa dhana mbalimbali za mada za *Fasihi Simulizi, Matumizi ya Lugha, Aina za Maneno, Usimulizi, Uandishi* na *Uundaji wa Maneno* zilizopimwa katika swali hili. Uchambuzi zaidi kuhusu namna wanafunzi walivyojibu vipengele mbalimbali vya swali hili umefafanuliwa kama ifuatavyo:

*(i) Seti ipi ni sahihi kuhusu vipengele vya fani katika fasihi simulizi?*

*A Dhamira, migogoro, mtindo na mafunzo.*
*B Ujumbe, matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na muundo.*
*C Wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari.*
*D Migogoro, ujumbe, wahusika, mafunzo na mtindo.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa kukumbuka vipengele vya fani katika fasihi simulizi. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi C *Wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari*; ambayo ni seti sahihi ya vipengele vya fani katika fasihi simulizi. Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vipengele vya fani katika fasihi simulizi.

Baadhi ya wanafunzi walishindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele hiki hivyo kuchagua vipotoshi A *Dhamira, migogoro, mtindo na mafunzo;* B *Ujumbe, matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na muundo;* na D *Migogoro, ujumbe, wahusika, mafunzo na mtindo.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na kukosa uelewa wa kutosha wa vipengele anuwai vya fani katika fasihi simulizi kwani ndani ya kila seti kulikuwa na mchanganyiko wa vipengele vya fani na maudhui. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuelewa kuwa dhamira, migogoro, mafunzo na ujumbe ni *mawazo, ukinzani* na *mafundisho* yatolewayo na mtunzi wa kazi za fasihi kwa lengo la kuwasilisha maudhui kwa jamii lengwa wakati *muundo, mtindo, matumizi ya lugha, mandhari* na *wahusika* kuwa ni vipengele vya fani vinavyoonesha namna ya uwasilishaji au ufikishaji wa mawazo ya mtunzi wa kazi ya fasihi kwa hadhira kusudiwa.

*(ii) Ni muundo upi wa ushairi wa fasihi simulizi unaundwa na mistari/mishororo mitano?*

*A Sabilia*
*B Takhmisa*
*C Tathmisa*
*D Tathilitha*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka miundo ya ushairi wa fasihi simulizi unaoundwa na mistari/mishororo mitano. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi kipengele hiki walichagua herufi B *Takhmisa* yaani shairi linaloundwa kwa mistari/mishororo mitano. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya miundo ya ushairi wa fasihi simulizi.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walionekana kukosa uelewa huo maana walichagua vipotoshi A *Sabilia*, C *Tathmisa* na D *Tathilitha*. Uchaguzi wa kipotoshi A *Sabilia* ulitokana na wanafunzi kukosa maarifa kuhusu aina ya shairi lisilokuwa na kibwagizo ambapo kituo au mshororo wake hubadilika kutoka ubeti hadi ubeti. Kipotoshi C *Tathmisa* ni aina ya ushairi wenye

muundo wa mistari miwili na D *Tathilitha* ni aina ya ushairi wenye muundo wa mistari mitatu.

*(iii) Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yana athari chanya na hasi katika ukuaji wa fasihi simulizi. Zipi ni athari hasi zinazoikabili fasihi simulizi?*

*A Hupunguza hadhi na ubora wa kazi za fasihi.*
*B Huhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa muda mrefu.*
*C Huboresha uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi.*
*D Hutunza kiini au maana ya ujumbe wa fasihi simulizi.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima maarifa ya mwanafunzi na uwezo wa kutathmini athari hasi za sayansi na teknolojia zinazoikabili fasihi simulizi. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi A *Hupunguza hadhi na ubora wa fasihi simulizi* kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uhai wa fasihi simulizi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliofanya upimaji huu walichagua vipotoshi B *Huhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa muda mrefu*, C *Huboresha uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi* na D *Hutunza kiini au maana ya ujumbe wa fasihi simulizi*; ambazo kwa ujumla ni athari chanya za sayansi na teknolojia katika ukuaji wa fasihi simulizi.

*(iv) Sababu zifuatazo husababisha kutokea kwa utata katika tungo,* ***isipokuwa:***

*A Neno kuwa na maana zaidi ya moja.*
*B Kuzingatia taratibu za uandishi.*
*C Kutumia maneno yenye maana ya picha.*
*D Kutotamka neno ulilokusudia kwa usahihi.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutambua sababu za kutokea kwa utata katika tungo. Wanafunzi waliokuwa na maarifa na uelewa wa kutosha walichagua herufi ya jibu sahihi B *Kuzingatia taratibu za*

*uandishi;* ambayo siyo sababu ya utata katika tungo bali huzuia/huondoa utata katika tungo.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali hili walichagua vipotoshi A *Neno kuwa na maana zaidi ya moja*; C *Kutumia maneno yenye maana ya picha*; na D *Kutotamka neno ulilokusudia kwa usahihi.* Wanafunzi hao walionesha kukosa uelewa wa kutosha kuhusu sababu za kutokea ama kuzuia utata katika tungo.

*(v) Juma huimba vizuri* <u>*sana*</u>*. Neno lililopigiwa mstari linafanya kazi ipi ya neno?*

*A Kielezi*
*B Kivumishi*
*C Kitenzi*
*D Kihisishi*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno,* mada ndogo ya *Ubainishaji wa Aina za Maneno* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutambua aina za maneno katika tungo. Wanafunzi waliojibu vyema swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi A *Kielezi* kwani walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za maneno katika lugha ya Kiswahili, hivyo kubainisha kwa usahihi neno **sana** kama *kielezi* ambalo ni neno au vifungu vya maneno ambavyo hufanya kazi ya kutoa maelezo au habari zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi au vielezi vingine.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walionesha kukosa uelewa kuhusu vielezi na aina za maneno kwa ujumla walichagua vipotoshi B *Kivumishi*, C *Kitenzi* na D *Kihisishi* kutokana na kushindwa kutambua dhima ya neno **sana** katika tungo waliyopewa. Uchaguzi wa kipotoshi B *Kivumishi* ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kutambua kazi ya kivumishi katika tungo ambayo ni kuelezea zaidi nomino au jina lilivyo. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi C *Kitenzi,* ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kubaini kazi za kitenzi katika tungo ambayo ni kuonesha tendo linalofanyika/lilofanyika/litakalofanyika. Pia, uchaguzi wa kipotoshi D *Kihisishi* ulitokana na wanafunzi hao

kushindwa kuelewa kuwa kihisishi ni neno linaloonesha hisia au mguso na vionjo vya moyo.

*(vi) Wewe na rafiki yako mmepewa kazi ya kubainisha sentensi yenye vivumishi vya **a- unganifu** katika tungo. Je, sentensi ipi kati ya zifuatazo itakuwa sahihi?*

*A Juma anacheza kwa madoido.*
*B Halima mrefu amefika.*
*C Abdul na Zuberi wameondoka jana.*
D *Janeth wa Dodoma ameingia darasani*.

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno,* mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina za Maneno* na lililenga kupima maarifa ya mwanafunzi katika kubainisha matumizi sahihi ya aina za maneno katika tungo. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi D *Janeth wa Dodoma ameingia darasani*. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vivumishi vya a- unganifu ambavyo huambatana na nomino au kiwakilishi.

Kwa upande mwingine, wapo wanafunzi waliokosa uelewa wa vivumishi vya a-unganifu, hivyo kuchagua vipotoshi A *Juma anacheza kwa madoido*, B *Halima mrefu amefika* na C *Abudul na Zuberi wameondoka jana*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa wanafunzi hao walishindwa kutambua matumizi sahihi ya maneno mbalimbali katika tungo.

*(vii) Kati ya kanuni zifuatazo, mojawapo **si** sahihi kuhusu usimulizi wa matukio.*

*A Kutamka matamshi kwa usahihi.*
*B Mpangilio mzuri wa mawazo.*
*C Kujua muundo wa tukio.*
*D Kutumia lugha kwa usahihi.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Usimulizi* na mada ndogo ya *Usimuliaji wa Matukio* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa kanuni za usimulizi wa matukio. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya

jibu sahihi C *Kujua Muundo wa Tukio* kuwa siyo kanuni stahiki kwa ajili ya usimulizi wa matukio.

Wanafunzi walioshindwa kujibu swali hili walichagua vipotoshi A *Kutamka matamshi kwa usahihi*; B *Mpangilio mzuri wa mawazo;* na D *Kutumia lugha kwa usahihi.* Uchaguzi wa vipotoshi A, B na D ulitokana na wanafunzi kukosa umahiri katika usimulizi wa matukio, hivyo kuchagua baadhi ya kanuni ambazo ni muhimu kuzingatiwa katika usimuliaji wa matukio kinyume na matakwa ya swali.

*(ix) Ipi ni dhima sahihi ya kutumia picha na michoro katika kamusi?*

*A Hufanya kamusi kutambulika kwa haraka.*
*B Hufanya kamusi kupendwa na wasomaji.*
*C Hupunguza umakini na idadi ya watumiaji.*
*D Huwasaidia wasomaji kuwa na kumbukumbu.*

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutambua dhima ya matumizi ya picha na michoro katika kamusi. Wanafunzi waliokuwa na umahiri katika swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi D *Husaidia wasomaji kuwa na kumbukumbu*; ambayo ndiyo dhima kuu ya kutumia picha na michoro katika kamusi.

Hata hivyo, kulikuwa na wanafunzi walioshindwa kubaini matumizi sahihi ya picha na michoro katika kamusi kwa kuchagua vipotoshi A *Hufanya kamusi kutambulika kwa haraka;* B *Hufanya kamusi kupendwa na wasomaji;* na C *Hupunguza umakini wa idadi ya watumiaji*. Kwa ujumla majibu yaliyopo katika vipotoshi hayakuwa na uhalisia na matumizi ya picha na michoro katika kamusi ambayo hulenga kumsaidia mtumiaji wa kamusi kupata maana za maneno ya lugha husika ili kujenga kumbukumbu ya maneno hayo. Hii ilitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa kutosha kuhusu kazi ya picha na michoro katika kamusi.

(x) *Ipi ni maana sahihi ya shina la neno kati ya zifuatazo ?*

*A Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali na tamati.*

*B Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali pekee.*

*C Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati pekee.*

*D Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati vijenzi.*

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutambua maana mbalimbali za maumbo yanayodhihirika katika kitenzi hususani shina la neno. Wanafunzi waliokuwa na umahiri kuhusu shina la neno walichagua herufi ya jibu sahihi C *Sehemu ya neno yenye mzizi na kiambishi tamati pekee*, ambayo ndiyo maana ya msingi ya shina la neno.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliojibu swali hili walishindwa kubaini maana sahihi ya shina la neno, hivyo kuchagua vipotoshi A *Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali na tamati*; B *Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali pekee;* na D *Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati vijenzi.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi kushindwa kutambua kuwa maana zilizopo katika vipotoshi hivyo zinahusu dhana ya unyumbulishaji/uambishaji katika kitenzi. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele (i) - (x) vya swali hili, hivyo kupata 0.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Seti ipi ni sahihi kuhusu vipengele vya fani katika fasihi simulizi?
A Dhamira, migogoro, mtindo na mafunzo.
B Ujumbe, matumizi ya lugha, wahusika, mtindo na muundo.
C Wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari.
D Migogoro, ujumbe, wahusika, mafunzo na mtindo.

[ B ]

(ii) Ni muundo upi wa ushairi wa fasihi simulizi unaundwa na mistari/mishororo mitano?
A Sabilia B Takhmisa
C Tathmisa D Tathilitha

[ C ]

(iii) Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yana athari chanya na hasi katika ukuaji wa fasihi simulizi. Zipi ni athari hasi zinazoikabili fasihi simulizi?
A Hupunguza hadhi na ubora wa kazi za fasihi.
B Huhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa muda mrefu.
C Huboresha uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi.
D Hutunza kiini au maana ya ujumbe wa fasihi simulizi.

[ B ]

(iv) Sababu zifuatazo husababisha kutokea kwa utata katika tungo, **isipokuwa**:
A Neno kuwa na maana zaidi ya moja.
B Kuzingatia taratibu za uandishi.
C Kutumia maneno yenye maana ya picha.
D Kutotamka neno ulilokusudia kwa usahihi.

[ D ]

(v) Juma huimba vizuri sana. Neno linalopigiwa msitari linafanya kazi ya aina ipi ya neno?
A Kielezi B Kivumishi
C Kitenzi D Kihisishi

[ C ]

(vi) Wewe na rafiki yako mmepewa kazi ya kubainisha sentensi yenye vivumishi vya ***a-unganifu*** katika tungo. Je, ni sentensi ipi kati ya zifuatazo itakuwa sahihi?
A Juma anacheza kwa madoido.
B Halima mrefu amefika.
C Abdul na Zuberi wameondoka jana.
D Janeth wa Dodoma ameingia darasani.

[ A ]

(vii) Kati ya kanuni zifuatazo mojawapo **si** sahihi kuhusu usimulizi wa matukio.
A Kutamka matamshi kwa usahihi.
B Mpangilio mzuri wa mawazo.
C Kujua muundo wa matukio.
D Kutumia lugha kwa usahihi.

[ B ]

(ix) Ipi ni dhima sahihi ya kutumia picha na michoro katika kamusi?
A Hufanya kamusi kutambulika kwa haraka.
B Hufanya kamusi kupendwa na wasomaji.
C Hupunguza umakini na idadi ya watumiaji.
D Husaidia wasomaji kuwa na kumbukumbu.

[ B ]

(x) Ipi ni maana sahihi ya shina la neno kati ya zifuatazo?
A Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali na tamati.
B Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi awali pekee.
C Sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi tamati pekee.
D Sehemu ya neno yenye mzizi na kiambishi tamati vijenzi.

[ A ]

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Katika kielelezo Na. 1.2, mwanafunzi alishindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote kutokana na kukosa uelewa kuhusu

dhana anuwai zilizopimwa katika mada mbalimbali katika kipengele (i) hadi (x).

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kutambua aina na dhima za nyimbo za fasihi simulizi. Swali liliuliza:

*Oanisha dhima za nyimbo za fasihi simulizi zilizo katika Orodha A na aina za nyimbo kutoka Orodha B kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku.*

| Orodha A | | Orodha B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Nyimbo zinazoimbwa ili kuburudisha watu. | A | Nyiso |
| | | B | Kimai |
| (ii) | Nyimbo za kuaga mwaka. | C | Bembezi |
| (iii) | Nyimbo zinazoimbwa kwenye maombolezo kama misiba. | D | Mbolezi |
| | | E | Tumbuizo |
| (iv) | Nyimbo zinazoimbwa kwenye shughuli za kilimo. | F | Wawe |
| | | G | Kongozi |
| (v) | Nyimbo zinazoimbwa kwenye jando na unyago. | | |

Swali lilikuwa na jumla ya vipengele vitano ambapo mwanafunzi alitakiwa kuoanisha dhima za nyimbo za fasihi simulizi zilizokuwa katika orodha A na aina za nyimbo hizo kutoka orodha B.

Wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo asilimia 75.31 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2.*

Chati Na. 2 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi ambapo wanafunzi 110,285 (17.37%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 3.5 hadi 5, wanafunzi 367,807 (57.94%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3 na wengine 156,751 (24.69%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 1.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi (57.94%) walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kuwa na maarifa yasiyojitosheleza kuhusu dhima za nyimbo za fasihi simulizi hivyo kuoanisha kwa usahihi vipengele 2 hadi 3 vya swali na kushindwa kuoanisha vipengele vingine. Wanafunzi hao walishindwa kubaini baadhi ya dhana zinazowakilisha dhima za nyimbo za fasihi simulizi. Majibu ya wanafunzi hao yalionesha kuwa, baadhi yao walichanganya dhima za nyimbo husika hususani nyimbo zinazoimbwa kwenye misiba (mbolezi) na zile zinazoimbwa kwa ajili ya kuaga mwaka (kongozi). Kwa ujumla, majibu ya wanafunzi katika vipengele hivyo hayakuwa ya kutosheleza, hivyo wakapata alama 1.5 hadi 3.

Wanafunzi wachache (17.37%) walipata ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu nyimbo ambazo ni kipera cha utanzu wa ushairi wa fasihi simulizi. Kutokana na umahiri huo, wanafunzi hao walioanisha kwa usahihi dhima za nyimbo za fasihi simulizi

katika *Orodha A* na aina za nyimbo husika katika *Orodha B* na kupata alama za juu katika swali hili. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote (5).

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | E | G | D | F | A |

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2.*

Katika kielelezo Na. 2.1, mwanafunzi alioanisha kwa usahihi dhima za nyimbo za fasihi simulizi katika Orodha A na aina ya wimbo kutoka Orodha B.

Hata hivyo, asilimia 24.69 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kuoanisha dhima za nyimbo na aina ya wimbo katika vipengele vingi vya swali hili na wengine walishindwa kuoanisha kipengele hata kimoja. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao ulionesha kuwa hawakuwa na umahiri kuhusu dhima mbalimbali za nyimbo kama kipera cha ushairi uliopo katika utanzu wa fasihi simulizi. Kwa ujumla, wanafunzi hao walishindwa kubaini dhima anuwai za nyimbo za fasihi simulizi kama vile: tumbuizo - *nyimbo zinazoimbwa ili kuburudisha watu*; kongozi - *nyimbo za kuaga mwaka*; mbolezi - *nyimbo zinazoimbwa kwenye maombolezo kama misiba*; wawe - *nyimbo zinazoimbwa kwenye shughuli za kilimo* na nyiso - *nyimbo zinazoimbwa kwenye jando na unyago*. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili na kupata 0.

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | D | C | G | A | F |

Kielelezo Na. 2.2: *Sampuli ya Majibu yasiyo sahihi katika Swali la 2.*

Katika Kielelezo Na. 2.2, mwanafunzi alishindwa kuoainisha dhima za nyimbo za fasihi simulizi katika Orodha A na aina ya nyimbo kutoka Orodha B kwa vipengele vyote na kupata 0.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba (7) yaliyokuwa ya majibu mafupi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 70 ambapo kila swali lilikuwa na alama 10. Maswali yaliyopimwa katika sehemu hii yalitungwa kutoka kwenye mada za *Ufahamu, Uundaji wa Maneno, Aina za Maneno, Mawasiliano, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Fasihi Simulizi* na *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi.*

### 2.2.1 Swali la 3: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* katika mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma Kimya* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka. Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari alichopewa kisha kujibu maswali katika vipengele vinne kuanzia (a) hadi (d). Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa.

*Baba mmoja aliishi na mkewe na mwanae wa pekee. Baba huyu alikuwa mtu wa kufuata maadili, mila na desturi za kiafrika. Alitamani kila mmoja ndani ya nyumba aishi maisha ya kimalaika. Hakupenda mtu nyeyote kwenda kinyume na mawazo yake ili maisha yake yasiende* ***mrama****, hasa mwanae aliyekuwa* ***mboni ya jicho lake****.*

*Binti yule akawa mtoto wa* ***getikali****, hakuna cha disko wala ufukweni. Mama yake naye hakuruhusiwa kujipamba kiasi cha kupitiliza, ikiwemo kusuka nywele kwa mitindo ya kisasa. Mama na binti yake walilazimika kutii kwa kumuogopa baba yule wa* ***miraba minne****, mwenye kuongea kwa mrindimo.*

*Siku moja binti yake aliwaza na kuwazua, akabaini kwamba pale nyumbani hapakuwa na maisha aliyoyahitaji, akaamua kufanya uamuzi mbaya wa kutoroka usiku. Baba na mama hawakujua mtoto alikokwenda. Mama akashikwa na* ***kihoro*** *akaumwa sana hatimaye umauti ukamfika.*

*Baba akasikitika sana, akatafakari na kutafakuri, hatimaye akagundua kuwa msimamo wake haukuwa sahihi na kwamba alitakiwa kupokea mawazo na kusikiliza ushauri toka kwa wengine. Vilevile akagundua kuwa hakuna mtu aliye mkamilifu kwani binadamu wote tuna upungufu.*

Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kupendekeza kichwa cha habari kinachoifaa habari aliyosoma na kisichozidi maneno matano. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kueleza maana ya maneno/vifungu vya maneno vifuatavyo kama vilivyotumika katika habari aliyosoma *(i) Mrama, (ii) Mboni ya jicho lake, (iii) Getikali, (iv) Miraba minne* na *(v) Kihoro.* Kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi; (i) kutoa sababu za uamuzi wa binti yule kutoroka nyumbani kwao na (ii) kuelezea tabia ya baba wa familia. Aidha, katika kipengele (d) mwanafunzi alitakiwa kuandika funzo linalopatikana kwenye habari aliyosoma.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya waliofanya upimaji katika somo hili. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri sana kwani asilimia 91.55 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3.*

Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi ambapo wanafunzi 212,128 (33.41%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 369,079 (58.14%) walifaulu

kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wengine 53,636 (8.45%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Kati ya wanafunzi waliojibu vizuri swali hili, 369,079 sawa na asilimia 58.14 walipata alama za wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kujibu vipengele (a) na (b) kwa usahihi kwa kupendekeza kichwa cha habari ATHARI ZA BABA MKALI ambacho kilisadifu vizuri kifungu cha habari kama ilivyotarajiwa katika (a) na kueleza maana ya maneno/vifungu vya maneno kama vilivyotumika katika habari aliyosoma kama vile (i) mrama - *kwenda vibaya*; (ii) mboni ya jicho lake - *mtoto wa pekee/tegemeo pekee*, (iii) getikali - *kufungiwa ndani bila ya kutoka nje*; (iv) miraba minne - *mtu mwenye nguvu*; na (v) kihoro – *huzuni/sononeko kubwa*. Pia, mwanafunzi huyo aliandika katika (c) (i) *Binti yule alitoroka nyumbani kutokana na ushawishi wa rafiki yake* na (ii) *baba wa familia hii alikuwa mwoga kwa mkewe na mwanae*, majibu yasiyojitosheleza, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 212,843 sawa na asilimia 33.41 walijibu vizuri swali hili, hivyo kupata alama za juu (6.5 hadi 10) kutokana na kukielewa vizuri kifungu cha habari walichopewa. Kati yao, asilimia 1.2 walipata alama zote (10) kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi maswali katika vipengele vyote ambapo katika kipengele (a) walipendekeza kichwa sahihi cha habari KILA MTU ANAHITAJI UHURU/HAKUNA MWANADAMU MKAMILIFU/ATHARI ZA UKALI KATIKA MALEZI/ ATHARI ZA BABA MKALI. Katika kipengele (b) walieleza maana za maneno (i) *mrama* - enda kombo, ovyo, vibaya, isivyo; (ii) *mboni ya jicho lake* - mtoto wake wa pekee/aliyepewa zawadi na Mungu, zawadi ya pekee, tegemeo pekee; (iii) *geti kali* - kufungiwa ndani/kutopewa ruhusa ya kutoka nje ya nyumba; (iv) *miraba minne* - mtu aliyejengeka na mwenye nguvu/pande la mtu; na (v) *kihoro* - huzuni kubwa kutokana na kufikwa na jambo la huzuni au kupotelewa na mali/mtu/sononeko kubwa/msongo. Katika kipengele (c) (i) walibaini kwa usahihi sababu za binti kutoroka nyumbani kwao

kuwa baba yake hakumpa uhuru wa kufanya lolote*;* na (c) (ii) alikuwa dikteta/mwenye msimamo mkali/mtu asiyetaka ushauri/anayetaka lifanywe lile analosema bila ya kupingwa. Pia katika kipengele (d) waliandika funzo linalopatikana katika habari waliyosoma kwa usahihi kuwa ni vizuri kusikiliza mawazo/ushauri wa watu wengine. Malezi bora si kuwafungia watoto ndani bali kuwafundisha ubaya/uzuri wa mambo ili wajue jinsi ya kuyaepuka/kuyafanya. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.

BABA WA SHERIA KALI

(b) Eleza maana ya maneno/vifungu vya maneno vifuatavyo kama vilivyotumika katika habari uliyosoma.

(i) Mrama

Kuharibika kwa jambo

(ii) Mboni ya jicho lake

- Tegemeo Lake

(iii) Geti kali

- Ni sehemu ambapo ni vigumu kutoka na sio rahisi kupata uhuru

(iv) Miraba minne

- Mtu mwenye nguvu

(v) Kihoro

Hali ya kuwa na hofu:

(c) (i) Unadhani kwa nini yule binti aliamua kutoroka nyumbani kwao?

Binti aliamua kutoroka nyumbani kwao kwa sababu nyumbani kwao hapakuwa na maisha aliyohitaji.

(ii) Baba wa familia hii alikuwa na tabia gani?

Baba wa familia alikua na tabia ya kuwanyima uhuru mke wake pamoja na binti yake

(d) Andika funzo linalopatikana katika habari hii.

Tusifanye mambo pasipo kufikiria maana huweza kuwababisha matatizo.

Kielelezo Na. 3.1*: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mwanafunzi alijibu vizuri vipengele vyote vitano kwa kuandika katika (a) kichwa cha habari kwa herufi kubwa na kisichozidi maneno matano, (b) maana sahihi za maneno/vifungu vya maneno aliyopewa kama yalivyotumika katika habari, (c) (i) sababu ya binti kutoroka nyumbani kwao, (ii) tabia ya baba wa familia na (d) funzo linalopatikana katika habari aliyosoma.

Licha ya swali hilo kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, wanafunzi 53,636 sawa na asilimia 8.45, walikuwa na ufaulu hafifu kutokana na kushindwa kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Kati yao, asilimia 1.0 walishindwa kujibu kipengele hata kimoja na kupata 0. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa uelewa wa kifungu cha habari walichopewa, badala yake baadhi walitoa majibu yasiyolandana na kifungu cha habari na wengine walinakili baadhi ya sentensi ndani ya kifungu cha habari na kuziandika kama majibu bila kuzingatia msingi wa swali lililoulizwa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele (a) aliandika kichwa cha habari kuwa ni *Mboni ya jicho lake* (b) (i) *mrama* kuwa ni *mwanae aliyekuwa mboni ya jicho lake; (ii) mboni ya jicho lake - binti yule akawa getikali hakuna cha disko wala ufukweni (iii) geti kali* kuwa ni *hakuna cha disko wala ufukweni;* (iv) *miraba minne - mwenye kuongea kwa mrindimo* (v) *kihoro - kuumwa sana hatimaye umauti ukamfika*. Pia, mwanafunzi huyo katika (c) (i) aliandika sababu sahihi ya binti kutoroka nyumbani kwao kuwa ni *kutofurahia maisha ya nyumbani kwao*; lakini katika kipengele (c) (ii) alinukuu baadhi ya sentensi zilizopo kwenye aya ya kwanza. Aidha, mwanafunzi huyo katika kipengele (d) alieleza funzo sahihi linalopatikana katika habari kuwa, *hakuna mtu aliye mkamilifu kwani binadamu wote tuna upungufu*. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama hafifu.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.

Baba mmoja aliishi na mkewe na mwanae wa pekee wa kike.

(b) Eleza maana ya maneno/vifungu vya maneno vifuatavyo kama vilivyotumika katika habari uliyosoma.

(i) Mrama

Hakupenda mtu yeyote kwenda kinyume na mawazo yake ili maisha yake yasiende mrama.

(ii) Mboni ya jicho lake

Hakupenda mtu yeyote kwenda kinyume na mawazo yake ili maisha yake yasiende mrama

(iii) Geti kali

Hakuna cha disko wala ufukweni.

(iv) Miraba minne

Mwenye kuongea kwa ndindimo.

(v) Kihoro

Akaumwa sana hatimaye umaiti ukampika.

(i) Unadhani kwa nini yule binti aliamua kutoroka nyumbani kwao?

Binti yule akawa mtoto wa geti kali, hakuna cha disko wala ufukweni. Alitamani kila mmoja ndani ya nyumba aishi maisha ya ~~kimalaika~~ kimalaika

(ii) Baba wa familia hii alikuwa na tabia gani?

Baba huyu alikuwa mtu wa kufuata maadili. mila na desturi za kiafrika.

Andika funzo linalopatikana katika habari hii.

Baba alisikitika sana akatafakari na kutafakari, hatimaye akagundua kuwa misimamo wake haukuwa sahihi na kuamba alitakiwa kupokea mawazo na kuakili za ushauri toka wengine.

Kielelezo Na. 3.2: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 3.*

Katika kielelezo Na. 3.2, mwanafunzi alijibu vipengele vya maswali kwa kunakili vifungu vya maneno kama yalivyoandikwa katika kifungu cha habari kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kuelewa kauli mbalimbali za vitenzi. Swali lilimtaka mwanafunzi kubainisha umbo linalodhihirisha kauli katika maneno aliyopewa kisha kutaja kauli husika kwa kila neno.

Swali lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Hili ni miongoni mwa

maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ambapo wanafunzi 403,473 sawa na asilimia 63.56 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 4:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4.*

Chati Na. 4 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi ambapo wanafunzi 61,449 (9.68%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 342,024 (53.88%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wengine 231,370 (36.44%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya wanafunzi (342,024) sawa na asilimia 53.88 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwani waliweza kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Aidha, wengine walibainisha maumbo sahihi ya kauli katika vitenzi walivyopewa, lakini wakashindwa kutaja kauli zinazowakilishwa na maumbo hayo na kinyume chake, hivyo kupata alama hafifu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele (a) wanapigana (i) umbo la kauli -*a*- badala ya –an- (ii) *kauli ya kutendeana*, (b) atatusomesha (i) umbo la kauli –*an*- badala ya –esh- (ii) *kauli ya kutendesha*; (c) limelimwa (i) umbo la kauli –*e*- badala ya –*w*- (ii) *kauli ya kutendwa* (d) amechomewa (i), umbo la kauli–*e*- badala ya -ew- (ii) *kauli ya*

*kutendewa* na (e) amepigika (i) umbo la kauli -*i*- badala ya -ik- (ii) *kauli ya kutendeka*. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa mwanafunzi hakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu kauli mbalimbali za vitenzi hivyo kushindwa kutofautisha umbo mahsusi la kauli katika vitenzi alivyopewa na kupata alama za wastani.

Wanafunzi wachache (61,449) sawa na asilimia 9.68 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya uundaji wa maneno. Wanafunzi hao waliweza kubainisha kwa usahihi maumbo yanayodhihirisha kauli katika maneno waliyopewa, kisha kutaja kwa usahihi kauli husika katika vipengele karibu vyote. Majibu sahihi ya wanafunzi hao yalikuwa katika kipengele (a) (i) umbo ni -*an*- na (ii) *kauli ya kutendana;* (b) (i) umbo ni -*esh*- na (ii) *kauli ya kutendesha*; (c) (i) umbo ni -*w*- na (ii) *kauli ya kutendwa;* (d) (i) umbo ni -*ew*- na (ii) *kauli ya kutendewa;* na (e) (i) umbo ni -*ik*- na (ii) *kauli ya kutendeka*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote 10.


(a) Wanapigana
(i) Umbo la kauli ... -an-
(ii) Kauli yenyewe ... kauli ya kutendana

(b) Atatusomesha
(i) Umbo la kauli ... -esh-
(ii) Kauli yenyewe ... kauli ya kutendesha

(c) Limelimwa
(i) Umbo la kauli ... -w-
(ii) Kauli yenyewe ... kauli ya kutendwa

(d) Amechomewa
(i) Umbo la kauli ... -ew-
(ii) Kauli yenyewe ... kauli ya kutendewa

(e) Amepigika
(i) Umbo la kauli ... -ik-
(ii) Kauli yenyewe ... kauli ya kutendeka

Kielelezo 4.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4.*

Katika kielelezo Na. 4.1, mwanafunzi alibainisha kauli katika vitenzi alivyopewa na kutaja kauli husika kwa kila neno kwa

usahihi, hivyo kukidhi matakwa ya swali katika vipengele vyote vya swali hili na kupata alama za juu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 231,370 sawa na asilimia 36.44 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao walionesha kukosa uelewa kuhusu kauli za vitenzi na mada ya uundaji wa maneno kwa ujumla. Baadhi yao, walibainisha maumbo ya kauli za vitenzi kwenye vipengele vichache na kushindwa katika vipengele vingi. Wengine walifafanua maneno waliyopewa kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alifafanua neno katika kipengele (b) atatusomesha kwa kuandika, (i) *mwalimu ndiye atatusomesha*, na (ii) *mwalimu wa Kiswahili atatusomesha mwaka ujao*; majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Wanafunzi hao walitakiwa kubainisha umbo linalodhihirisha kauli na kutaja kauli husika katika maneno aliyopewa kama ifuatavyo: (a) (i) umbo ni -*an*- na (ii) *kauli ya kutendana;* (b) (i) umbo ni -*esh*- na (ii) *kauli ya kutendesha*; (c) (i) umbo ni -*w*- na (ii) *kauli ya kutendwa;* (d) (i) umbo ni -*ew*- na (ii) *kauli ya kutendewa;* na (e) (i) umbo ni -*ik*- na (ii) *kauli ya kutendeka*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubainisha umbo la kauli na kutaja kauli husika katika vipengele vyote na kupata 0.


(a) Wanapigana
(i) Umbo la kauli -a-
(ii) Kauli yenyewe kauli ya kutenda

(b) Atatusomesha
(i) Umbo la kauli -e-
(ii) Kauli yenyewe kauli ya kutendwa:

(c) Limelimwa
(i) Umbo la kauli -i-
(ii) Kauli yenyewe kauli ya kutendea:

(d) Amechomewa
(i) Umbo la kauli -e-
(ii) Kauli yenyewe kauli ya kutendwa:

(e) Amepigika
(i) Umbo la kauli -i-
(ii) Kauli yenyewe kauli ya kutendwa:

Kielelezo Na. 4.1: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.*

Katika kielelezo Na. 4.1, mwanafunzi alibaini umbo la kitenzi katika vipengele vyote kama –a-, -e- na -i- na kutaja kauli ya kutenda, kutendwa na kutendea kwa maumbo yote kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.3 Swali la 5: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina za Maneno*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuchambua aina za maneno na lilimtaka mwanafunzi kubainisha viwakilishi katika tungo alizopewa na kuonesha aina ya kiwakilishi husika kwa kila tungo.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 kati ya wote waliofanya upimaji wa somo hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu ambapo asilimia 93.85 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 39,012 | 6.15 |
| 3.0 - 6.0 | 262,474 | 41.34 |
| 6.5 - 10 | 333,357 | 52.51 |

**Jedwali Na. 2** linaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 52.51 walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 41.34 kiwango cha wastani, na asilimia 6.15 kiwango hafifu.

Wanafunzi 333,357 sawa na asilimia 52.51 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10 hadi 15. Ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi wengi walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada ya *Aina za Maneno* hivyo waliweza kubainisha kwa usahihi viwakilishi katika sentensi walizopewa kisha kuonesha aina ya kila kiwakilishi kama swali lilivyowataka. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibaini kwa usahihi viwakilishi na kuonesha aina ya kiwakilishi katika

vipengele vyote vya swali hili kama vile: (a) Yule hapendi ugali; (i) *Yule* na (ii) *kiwakilishi kionyesh*i; (b) Sisi tunapenda kusoma; (i) *Sisi* na (ii) *kiwakilishi cha nafsi*; (c) Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi; (i) *wako* na (ii) - *kiwakilishi cha umiliki*; (d) Wengi wamepokelewa vizuri; (i) *wengi* na (ii) *kiwakilishi cha idadi*; na (e) Mrefu wa kimo amefik*a*; (i) *mrefu* na (ii) *kiwakilishi cha sifa.* Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali.


5. Bainisha viwakilishi katika tungo zifuatazo na kwa kila moja onesha ni kiwakilishi cha aina gani.

**Mfano**: Hili limeoza.

(i) Kiwakilishi - hili.

(ii) Aina - kiwakilishi cha kuonesha.

(a) Yule hapendi ugali.

(i) Kiwakilishi......Yule......

(ii) Aina.......Kiwakilishi kionyeshi......

(b) Sisi tunapenda kusoma.

(i) Kiwakilishi.....Sisi......

(ii) Aina....Kiwakilishi cha nafsi......

(c) Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi.

(i) Kiwakilishi......wako......

(ii) Aina.....Kiwakilishi Kimilikishi......

(d) Wengi wamepokelewa vizuri.

(i) Kiwakilishi......Wengi......

(ii) Aina.....Kiwakilishi cha idadi......

(e) Mrefu wa kimo amefika.

(i) Kiwakilishi......Mrefu......

(ii) Aina......Kiwakilishi cha sifa......

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1, mwanafunzi alibainisha viwakilishi katika tungo (a – e) na kuonesha aina ya kiwakilishi husika kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali.

Wanafunzi 262,474 sawa na asilimia 41.34 ya wote waliojibu swali hili waliweza kubainisha viwakilishi na kuonesha ni vya aina gani kwa baadhi ya tungo, hivyo kupata alama za wastani

yaani 3 hadi 6 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika baadhi ya vipengele.

Aidha, wanafunzi wachache (39,012) sawa na asilimia 6.15 ya wote waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia 0 hadi alama 2.5 kutokana na kukosa uelewa kuhusu ufafanuzi wa aina za maneno kwa ujumla. Kutokana na kukosa umahiri huo, wanafunzi hao walishindwa kubainisha na kuonesha aina za viwakilishi kwa usahihi kama vilivyotumika kwenye tungo walizopewa katika vipengele 4 – 5. Baadhi ya wanafunzi katika kundi hili walitoa majibu yenye mkanganyiko kutokana na kuchanganya dhana za viwakilishi na vivumishi, na wengine kubainisha vitenzi. Hali kadhalika, wapo walioshindwa kuonesha kiwakilishi husika ni cha aina gani na badala yake walitaja aina nyinginezo za maneno kama vile viunganishi, vihisishi na vielezi kama aina za viwakilishi husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa majibu yafuatayo katika kipengele (a) *Yule hapendi ugali*; alibainisha (i) kiwakilishi *hapendi* badala ya ***yule*** (ii) aina - *kivumishi* badala ya kiwakilishi kionyeshi. (b) *Sisi tunapenda kusoma* (i) kiwakilishi - *tunapenda* badala ya **sisi** (ii) aina - *kihisishi* badala ya kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi*;* na kipengele (c) *Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi* (i) kiwakilishi - *amerudi* badala ya **wako** na (ii) aina - *kiwakilishi* badala ya kiwakilishi cha kumiliki. Vivyo hivyo, katika kipengele (d) *Wengi wamepokelewa vizuri* (i) kiwakilishi - *wamepokelewa* badala ya **wengi** na (ii) aina - *kihusishi* badala ya kiwakilishi cha idadi; na kipengele (e) *Mrefu wa kimo amefika* (i) kiwakilishi - kimo badala ya **mrefu** na (ii) aina - *kivumishi* badala ya kiwakilishi cha sifa. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama hafifu.


5. Bainisha viwakilishi katika tungo zifuatazo na kwa kila moja onesha ni kiwakilishi cha aina gani.

**Mfano**: Hili limeoza.

(i) Kiwakilishi - hili.

(ii) Aina - kiwakilishi cha kuonesha.

(a) Yule hapendi ugali.

(i) Kiwakilishi... Huyu. ...

(ii) Aina... Kiwakilishi Cha nafsi ...

(b) Sisi tunapenda kusoma.

(i) Kiwakilishi... Wale ...

(ii) Aina... Kiwakilishi Cha Idadi ...

(c) Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi.

(i) Kiwakilishi... Yule ...

(ii) Aina... Kiwalishi Cha Sifa ...

(d) Wengi wamepokelewa vizuri.

(i) Kiwakilishi... Wale. ...

(ii) Aina... Kiwakilishi Cha Sifa ...

(e) Mrefu wa kimo amefika.

(i) Kiwakilishi... Yule ...

(ii) Aina... Kiwakilishi Cha Idadi ...

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mwanafunzi alibainisha viwakilishi kimakosa katika tungo (a – e) kwa kutaja viwakilishi visivyokuwa katika tungo husika na kuonesha aina ya kiwakilishi hicho kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.4 Swali la 6: Dhima ya Lugha

Swali lilitoka katika mada *ya Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*, mada ndogo ya *Dhima ya Lugha.* Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua dhima mbalimbali za lugha kama chombo cha mawasiliano. Swali lilimtaka mwanafunzi kueleza dhima tano za lugha.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji katika somo hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha

ufaulu ambapo asilimia 59.07 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 5***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6.*

Chati Na. 5 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi ambapo wanafunzi 115,636 (18.22%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 259,421 (40.86%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wengine 259,786 (40.92%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Wanafunzi wengi 259,421 sawa na asilimia 40.82 waliofaulu katika swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kuanzia alama 3 hadi 6 kutokana na kueleza kwa usahihi baadhi ya dhima za lugha na kushindwa kutoa mifano dhahiri ili kutosheleza ufafanuzi wa hoja husika, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitaja kwa usahihi dhima mojawapo ya lugha kama utambulisho wa jamii lakini hakuonesha namna lugha inavyoweza kumtambulisha mtu anayetoka kwenye jamii nyingine. Wanafunzi wengine walitoa hoja pungufu kutokana na kurudia baadhi ya dhima zenye matumizi ya aina moja kama vile *chombo cha mawasiliano* na *chombo chenye kuleta maelewano baina ya watu*.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (115,636) sawa na asilimia 18.22 ndio waliokuwa na ufaulu mzuri wa alama 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa wa dhima za lugha kama vile: *utambulisho wa jamii*; *sehemu ya utamaduni wa watu*; *chombo cha kutolea elimu, chombo cha mawasiliano*; na *lugha kama chombo kinachoendeleza umoja na ushirikiano*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

6. Eleza dhima tano za lugha.

(a) Lugha ni sehemu ya utamaduni wa watu. Kwa sababu lugha inatumika na watu wa jamii mbalimbali na kila jamii ina lugha yake ambayo hutumiwa na watu wa eneo hilo.

(b) Lugha ni nyenzo ya kufundishia. Lugha inatumika kufundisha wanafunzi shuleni katika masomo mbalimbali mfano: Kiswahili na Kingereza hutumika shuleni.

(c) Lugha hutumika kama nyenzo ya kudhihirisha hisia. Kwa sababu lugha inaweza kudhihirisha hisia ya mtu kwa jinsi anavyoongea maneno yake. Mfano kwa upole au kwa ukali.

(d) Lugha ni utambulisho wa jamii. Lugha inaweza kutambulisha jamii kwa kutokana na lafudhi anayotumia mtu kuongea lugha anayotumia itaonyesha kuwa huyu mtu ni jamii gani.

(e) Lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano. Lugha inatumiwa na watu wote kwa ajili ya kuwasiliana au kupashana habari fulani katika maeneo mbalimbali.

Kielelezo Na. 6.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6.*

Katika kielelezo Na. 6.1, mwanafunzi alieleza kwa usahihi dhima zote tano za lugha na kukidhi matakwa ya swali.

Hata hivyo, wanafunzi 259,786 sawa na asilimia 40.92 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5 kutokana na kukosa umahiri katika mada ya *Mawasiliano* na kushindwa kueleza kwa usahihi dhima za lugha. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu vibaya swali hili kwa kuandika dhima zisizo sahihi kama vile: (a) *Kuwasiliana kwa simu,* (b) *Kuandika barua,* (c) *Kuwakilishwa kwenye mikutano,* (d) *Kusimulia hadithi*, na (e) *Kutumia fasihi*; majibu ambayo hayahusiani na dhima anuwai za lugha kama chombo cha mawasiliano. Kielelezo Na.

6.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata 0.


6. Eleza dhima tano za lugha.

(a) Hutusaidia kujua mila na desturi.

(b) Hutuaidia kutambua Utu mbalimbali katika jamii.

(c) Hutuaidia kujua nini maana ya Uituwingi Viliyo jificha

(d) Hutusaidia kufafanua Umoja na Wingi katika Lugha

(e) Hutusaidia kujua matamshi yaliyotam kwa katika hiyo Lugha.

Kielelezo Na. 6.2: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.2, mwanafunzi aliandika mambo mchanganyiko yasiyo na uhusiano wowote na dhima ya lugha kama chombo cha mawasiliano katika jamii na kupata 0.

### 2.2.5 Swali la 7: Sifa za Misimu

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Misimu*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa misimu mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Swali lilimtaka mwanafunzi kufafanua sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji katika somo hili. Swali hili ndilo lilikuwa na ufaulu wa kiwango cha chini zaidi ikilinganishwa na maswali yote yaliyopimwa kwani asilimia 43.97 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 6***: Ufaulu wa Wanafunzi kwa Asilimia katika Swali la 7.*

Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi ambapo asilimia 11.73 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, asilimia 33.24 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6, na asilimia 55.03 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Zaidi ya nusu ya wanafunzi (55.03%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walishidwa kufafanua sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili. Kati yao, asilimia 26.6 walipata 0 kwa kuwa walishindwa kabisa kufafanua sifa hata moja ya misimu katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi yao walibainisha aina za misimu kama vile *misimu tarafa*, *misimu zagao*, *misimu ya kipekee*, *misimu tegemezi* na *misimu huru* kinyume na matakwa ya swali. Wanafunzi wengine walitaja vipengele mbalimbali vya fani katika kazi za fasihi kama vile *matumizi ya lugha, muundo, mtindo, mandhari* na *wahusika*; mambo ambayo hayahusiani na sifa za misimu katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hao walitakiwa kufafanua sifa anuwai za misimu katika lugha ya Kiswahili kama vile *kuzuka na kupotea, kutumia maneno yasiyo rasmi, kupendwa sana na watu, kufurahisha/kuchekesha na kutumia lugha ya mafumbo.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali la 7.

7. Fafanua sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili.

(a) Hukuza lugha: Unapongea kiswahili hukuza lugha ya ~~kiswahili~~ katika jamii pia katika nchi mbalimbali pia lugha ya taifa lako huweza kukuza lugha.

(b) Huleta uelewano baina ya wa Africa: Unapongea lugha ya taifa lingine huwa hawawezi kukuelewa lakini unapongea kiswahili wote watajua.

(c) Kiswahili ni mali ya taifa zima; Takuwa kiswahili ni mali ya taifa dhima kwa kuwa mtu anapongea kiswahili anaelewa ukiongea lugha nyingine watakaojua ni wale tu wanao..

(d) Lugha husaidia kutengeneza misimu mbalimbali; Mfano mtu anapo sema neno jipya na likaleta maana huwa linatengeneza misimu mpya katika lugha ya kiswahili.

Kielelezo Na. 7.1: Sehemu ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Katika kielelezo Na. 7.1, mwanafunzi alieleza baadhi ya dhima za lugha ya Kiswahili ambazo sio sahihi kama vile *huleta uelewano* na *mali ya taifa* japo si dhahiri badala ya kufafanua sifa za misimu katika lugha ya Kiswahili.

Asilimia 33.24 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwani majibu yao yalionesha kuwa na mapungufu katika baadhi ya vipengele kwa kuwa walishindwa kufafanua sifa za misimu katika lugha ya Kiswahili, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walitaja sifa za misimu kwa usahihi lakini walitoa ufafanuzi usio sahihi kwa sifa walizobaini na wengine waliandika sifa za misimu bila kutoa maelezo zaidi kuhusu sifa hizo kama swali lilivyotaka.

Wanafunzi 74,482 sawa na asilimia 11.73 walijibu vizuri swali hili, na kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kufafanua sifa sahihi za misimu katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwao, asilimia 3.7 walipata alama zote (10) katika swali hili kutokana na kuonesha uelewa wa kutosha kuhusu sifa bainifu za misimu dhidi ya vipengele vingine anuwai vya matumizi ya lugha, hususani lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hao walifafanua kwa usahihi sifa tano za misimu katika lugha ya

Kiswahili kama vile: *huzuka kutokana na mabadiliko ya kihistoria yanayoikumba jamii husika; huwa ni maneno ya lugha isiyo sanifu; huwa na lugha ya mafumbo; huwa na chumvi nyingi; hupendwa na watu wengi;* na *huelimisha jamii*. Majibu hayo yalikidhi matakwa ya swali hili ipasavyo. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote.


7. Fafanua sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili.

(a) Misimu huzuka na hutumika katika kipindi fulani cha muda kulingana na matukio au matendo yanayotendeka wakati huo, mfano chakachua, lililotumika sana kipindi cha mwaka 2016

(b) Misimu hupotea na huacha kutumika pale hali husika katika jamii itakapotoweka. Msemaji au mtumiaji huacha kutumia misimu hiyo pale ambapo hali itakapotoweka, mfano, vyuma vimekaza.

(c) Misimu huweza kupandishwa hadhi na kusanifishwa na kuwa msamiati rasmi katika lugha iwapo itatumika kwa muda mrefu, mfano, daladala.

(d) Misimu inachuku nyingi na hutumia lugha au maneno yasiyo sanifu. Misimu hutumia maneno yasiyo sanifu ambayo huweza kutungwa kwa sababu ya hali au tukio fulani katika jamii.

(e) Misimu hupendwa sana na vijana na hupendezesha (yaani hupamba na hutia mvuto lugha). Misimu hupendwa sana na vijana katika jamii kwani huendana na matukio yanayoendelea.

Kielelezo Na. 7.2: *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.*

Katika kielelezo Na. 7.2, mwanafunzi alifafanua kwa usahihi sifa tano za misimu katika lugha ya Kiswahili pamoja na kutoa mifano dhahiri kwa kila hoja, hivyo kupata alama kumi (10).

### 2.2.6 Swali la 8: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Simulizi na mada ndogo ya Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutathmini mafunzo yanayopatikana katika methali alizopewa. Swali liliuliza:

*Ni mafunzo gani yanayopatikana katika methali zifuatazo ?*

*(a)* *Samaki mkunje angali mbichi.*

*(b)* *Mchumia juani hulia kivulini.*

*(c)* *Akiba haiozi.*

*(d)* *Safari ni hatua.*

*(e)* *Akili ni nywele kila mtu ana zake.*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo asilimia 66.60 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 8.*

Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 33.40 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama 0 hadi 2.5, asilimia 43.01 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6, na asilimia 23.59 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10.

Asilimia 33.40 ya wanafunzi waliojibu swali hili walishindwa kueleza mafunzo yanayopatikana katika methali walizopewa. Miongoni mwao, asilimia 17.1 walipata 0 kutokana na kukosa umahiri wa kutathmini mafunzo anuwai ya methali zilizo katika vipengele (a) – (e). Baadhi yao walitunga methali nyingine zinazokaribiana kimaana na methali walizopewa kinyume na

matakwa ya swali. Wengine waliandika kauli/maneno yasiyofungamana na methali husika kama vile miundo ya methali, vitendawili, misemo na nahau kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipegele (a) 'Samaki mkunje angali mbichi,' aliandika' *Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu* na *Acha mbachao kwa msala upitao*; (b) 'Mchumia juani hulia kivulini' - *Mchumia jangwa hula na wa kwao*; (c) 'Akiba haiozi' - *Siku ya mwizi ni arobaini*; (d) 'Safari ni hatua' - *mbio za sakafuni huishia ukingoni* na *Kuku mgeni akosi kamba mguuni*; na (e) 'Akili ni nywele kila mtu ana zake' - *Sikio la kufa halisikii dawa* na *Haraka haraka haina baraka*. Mwanafunzi huyo hakueleza mafunzo yoyote katika methali alizopewa bali aliandika methali zingine mbili kwa kila methali. Vilevile, aliandika methali kimakosa kwa kuandika *Acha mbachao kwa msala upitao* badala ya 'usiache mbachao kwa msala upitao.' Kwa ujumla, mwanafunzi huyu alionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya busara zinazojengwa katika methali ili ziweze kutoa mafunzo stahiki kwa jamii lengwa kama vile (a) *watoto wapewe malezi na maadili mema wakiwa wadogo kwa sababu wakiwa wakubwa itakuwa vigumu kuwabadilisha;* (b) *anayefanya kazi kwa bidii lazima atapata matunda/mafanikio ya kazi yake;* (c) *mwenye kuweka akiba itamsaidia hapo baadae wakati wa shida/uhitaji;* (d) *tunapotenda au kufanya jambo gumu tuwe na uvumilivu kwani litakamilika tu hatua kwa hatua;* na (e) *binadamu/watu wameumbwa wakiwa na tofauti nyingi*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali hili na kupata 0.


8. Ni mafunzo gani yanayopatikana katika methali zifuatazo?

(a) Samaki mkunje angali mbichi.

Samaki akikauka ukimkunja anavunjika.

(b) Mchumia juani hulia kivulini.

Mtu akizoea kukaa juani anakaa kivulini

(c) Akiba haiozi.

Ukihifadhi kitu kuamba utakitumiaga siku nyingine hakiozi au ukiweka mazao ndani ukiyatunza vizuri kuwa utapandaga msimu wa kupanda hayaozi.

(d) Safari ni hatua.

Unavozidi kutembea ndo unazidi kwenga mbele

(e) Akili ni nywele kila mtu ana zake.

Kila mtu anafanya ya kwake

Kielelezo Na. 8.1: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.1, mwanafunzi alifafanua methali alizopewa kwa kutumia tafsiri sisisi za maneno yaliyounda methali hizo badala ya kutathmini mafunzo yanayotolewa kwa kila methali kama ilivyotarajiwa.

Hata hivyo, wanafunzi 273,046 sawa na asilimia 43.01 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa mafunzo ya baadhi ya methali walizopewa. Aidha, walieleza kwa usahihi mafunzo yanayopatikana kwenye baadhi ya methali walizopewa na kushindwa katika methali zingine. Wengine walitoa maelezo yasiyojitosheleza katika kuelezea mafunzo yanayopatikana katika methali walizopewa na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwafunzi mmoja alieleza kwa usahihi mafunzo ya methali katika vipengele (a), (b) na (c) lakini alishindwa kueleza mafunzo katika methali (d) na (e) na kupata alama za wastani.

Wanafunzi wachache (149,778) sawa na asilimia 23.59 ndio walioweza kueleza kwa usahihi mafunzo yanayopatikana kwenye methali walizopewa. Baadhi yao, (3.9%) walionesha kuwa na umahiri wa juu wa mafunzo mbalimbali yaliyopo katika methali, hivyo waliweza kutathmini mafunzo katika methali walizopewa

kwa usahihi na kupata alama zote (10) za swali hili. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alieleza kwa usahihi mafunzo yanayopatikana katika methali alizopewa kama ifuatavyo: Kipengele (a) Samaki mkunje angali mbichi; kuwa *ni vyema ukamfunza maadili mema mtu akiwa bado mdogo kwani akishakuwa mtu mzima itakuwa ni ngumu kumbalisha*; (b) Mchumia juani hulia kivulini; kuwa *mtu anayefanya kazi kwa bidii, ugumu na kwa jasho baadae hupata matunda au mafanikio mazuri*; (c) Akiba haiozi; kuwa *ni vizuri kutunza vitu au mali kwani haviwezi kuharibika ila vitakusaidia utakapokuwa na shida navyo hapo baadae*, (d) Safari ni hatua; kuwa *kwa kila tunachokifanya ni lazima tupitie viwango au vipimo mbalimbali ndipo tuweze kufanikiwa au kufikia malengo tunayotarajia kuyatimiza*; na (e) Akili ni nywele kila mtu ana zake; kuwa *kila mtu huwa na akili tofauti na mwenzake hivyo mawazo na mitazamo hutofautiana baina ya watu*. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mwanafunzi aliyeeleza mafunzo stahiki katika methali zote alizopewa.

8. Ni mafunzo gani yanayopatikana katika methali zifuatazo?

(a) Samaki mkunje angali mbichi.

Maana yake Kirekebishe kitu kikiwa bado dogo ukiliacha baadaye ila kuwa ngumu kukirekebisha

(b) Mchumia juani hulia kivulini.

Ku Ukivumilia mateso ya muda baadaye utapata faraja.

(c) Akiba haiozi.

Maana: yake chochote utakachopata ujifunze kuweka akiba ili kikufae kesho au baadaye.

(d) Safari ni hatua.

Hii maana ya kila kitu unachotaka kufanya lazima uanze na hatua baada ya hatua ili kufikia lengo

Kielelezo Na. 8.2: *Sehemu ya majibu sahihi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.2, mwanafunzi alieleza kwa usahihi mafunzo mbalimbali yanayopatikana katika methali (a) – (d) na kupata alama za juu.

### 2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi.* Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa njia mbalimbali za kuhifadhi kazi za kifasihi. Swali lilimtaka mwanafunzi kufafanua njia tano za kuhifadhi kazi za fasihi.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji wa somo hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani asilimia 78.34 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 137,457 | 21.65 |
| 3.0 - 6.0 | 262,849 | 41.40 |
| 6.5 - 10 | 234,837 | 36.94 |

**Jedwali Na. 3** linaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 36.94 walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 41.40 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 21.65 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Wanafunzi 262,849 sawa na asilimia 41.40 waliojibu swali hili waliweza kufafanua baadhi ya njia za kuhifadhi kazi za fasihi kwa usahihi lakini walishindwa katika njia nyingine, hivyo kupata alama za wastani. Majibu yasiyojitosheleza ya wanafunzi katika swali hili yalitokana na baadhi yao kuchanganya baadhi ya njia kwa kuzirudia bila kutambua dhima zake kiuhalisia na kiutendaji. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibainisha njia ya *vinasa sauti* kwa usahihi lakini akataja pia *redio* ambayo hufanya

kazi pia kama kinasa sauti, hivyo kuwa na hoja pungufu na kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 234,457 sawa na asilimia 36.94 ya waliofanya upimaji huu walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia alama 6.5 hadi 10 kutokana na kuonesha uelewa wa kutosha wa njia za uhifadhi wa kazi za fasihi. Miongoni mwao, asilimia 15 walipata alama zote za swali kwani waliweza kufafanua kwa usahihi njia tano za uhifadhi wa kazi za fasihi kama vile: *kichwani, maandishi, vinasa sauti, kanda za video, kompyuta* na *mtandaoni*, hivyo kukidhi matakwa ya swali. Pia, wanafunzi hao walitoa mifano ya kazi mbalimbali za fasihi ambazo zimehifadhiwa kwa njia walizobaini na kueleza faida ama hasara za uhifadhi wa kazi za fasihi katika njia husika. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekidhi matakwa ya swali hili na kupata alama zote (10).


9. Kazi za fasihi huhifadhiwa kwa njia mbalimbali. Fafanua njia tano za kuhifadhi kazi hizo.

(a) Kichwani; hii ni njia ya kuhifadhi Fasihi kwa kurithi kutoka kwa Fanani aliyekuhadithia kazi hiyo kama ya Hadithi.

(b) Kompyuta; hii ni njia ya kuhifadhi Fasihi kwa kuiweka kwenye kifaa cha kisasa ambapo huweza kukaa kwa muda mrefu bila kupoteza labda kompyuta ikiharibika.

(c) Maandishi; hii ni njia ya kuhifadhi Fasihi kwa kuiweka katika mfumo wa maandishi katika vitabu au magazeti baada ya kusikiliza kwa umakini.

(d) Vinasa sauti; hii ni njia ya kuhifadhi Fasihi kwa kurekodi sauti yake wakati ilipokuwa ikisimuliwa kwa kuiweka kwenye Tepu rekoda.

(e) Kanda za Video; hii ni njia ya kuhifadhi Fasihi kwa kurekodi sauti pamoja na picha ya kazi ya fasihi. Njia hii huweza kudumu kwa muda mrefu.

Kielelezo Na. 9.1: *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.1, mwanafunzi alifafanua kwa usahihi njia tano za uhifadhi wa kazi za fasihi na kupata alama za juu katika swali hili.

Hata hivyo, wanafunzi wengine (137,457) sawa na asilimia 21.65 waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Miongoni mwao, asilimia 8.1 walipata 0 kwa kuwa walishindwa kabisa kufafanua njia walau moja ya kuhifadhi kazi za fasihi, kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu njia mbalimbali za uhifadhi wa kazi za fasihi kwa ujumla. Baadhi yao waliandika dhima za fasihi/kamusi kama vile: (a) *hukuza lugha kwa jamii*; (d) *huonya na kuelekeza jamii*; na (e) *huburudisha jami*. Katika kipengele (b) *huwa na msemaji na msikilizaji*; na kipengele (c) *huonesha matamshi sahihi ya neno*; wengine walifafanua tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi badala ya kufafanua njia tano za kuhifadhi kazi za fasihi kama vile *kichwani, maandishi, vinasa sauti, kanda za video, kompyuta* na *mtandaoni*. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kufafanua walau njia hata moja za kuhifadhi kazi za fasihi, hivyo kupata 0.


9. Kazi za fasihi huhifadhiwa kwa njia mbalimbali. Fafanua njia tano za kuhifadhi kazi hizo.

(a) Fasihi huokoa gharama
Fasihi huokoa gharama katika jamii kunanyingine haiokoi gharama

(b) Fasihi huokoa muda
fasihi huokoa muda sana kunanyingine huwa haziokoi muda

(c) Fasihi kuna kongwe na ambayo si kongwe.
fasihi kuna zile ambazo kongwe nanyingine nikongwe sana.

(d) Fasihi ha haiokoi gharama.
fasihi kuna hile ambayo inaokoa gharama katika fasihi.

(e) Fasihi inachukua muda mrefu.
Fasihi inaweza kukaa kwa mudamrefu sana

Kielelezo Na. 9.2: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.2, mwanafunzi aliandika dhana zinazotofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi katika vipengele vya *muda, gharama na umri* kinyume na matakwa ya swali.

## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU (INSHA)

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lililomtaka mwanafunzi kuandika insha ya hoja. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Uandishi wa Insha

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, na mada ndogo ya *Uandishi wa Insha za Hoja* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutathmini maswala mtambuka katika jamii. Swali lilimtaka mwanafunzi kuandika insha ya hoja kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200 kuhusu 'Umuhimu wa Michezo.'

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 634,843 kati ya wote waliopimwa katika somo hili. Ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri kwani asilimia 75.56 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 4 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 4: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 4.0 | 155,175 | 24.44 |
| 4.5 – 9.5 | 286,831 | 45.18 |
| 10.0 – 15.0 | 192,837 | 30.38 |

**Jedwali Na. 4** linaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 30.38 walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 45.18 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 24.44 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Wanafunzi 192,837 sawa na asilimia 30.38 walifaulu kwa kiwango kizuri. Ufaulu huo ulitokana na maarifa na ujuzi walio nao kuhusu uandishi wa insha za hoja. Wanafunzi hao waliweza kuandika insha yenye hoja nne (4) kuhusu umuhimu wa michezo kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha. Taratibu hizo ni pamoja na kuandika kichwa cha insha kwa herufi kubwa; utangulizi wa insha kwa kueleza maana ya michezo na aina za michezo; kiini cha insha chenye hoja zinazoelezea umuhimu wa

michezo kama vile; *hujenga afya, michezo hukuza urafiki, huingiza kipato, hutambulisha jamii/taifa, hutoa ajira kwa vijana, huleta furaha na burudani, huibua vipaji mbalimbali, na hujenga umoja na ushirikiano*. Pia, wanafunzi hao waliandika hitimisho lililoendana na hoja walizoandika. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

10. Kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200, andika insha yenye hoja nne kuhusu Umuhimu wa Michezo.

UMUHIMU WA MICHEZO

Michezo ni shughuli ziroazofanywa na watu ambazo hujumuisha kukimbia, kucheza mpira wa mikono, mpira wa kikapu, mpira wa miguu, kuruka kamba, rede, mashindano ya kuogelea na mengine mengi. Watu wengi hujishughulisha na michezo hii na watu wengine hawapendi kushiriki kwenye michezo sababu hawajui umuhimu wake. Hivyo basi vifuatavyo ni umuhimu wa michezo.

Michezo huimarisha afya ya yule anayeshiriki. Kwa kushiriki kwenye michezo ya mpira, kukimbia, kuogelea mtu anaimarisha afya yake kwa kuimarisha mifupa, kinga ya mwili na kupunguza mafuta mwili ambayo huleta matatizo ya afya kama vile kushtuka kwa moyo.

Kukuza ushirikiano, na umoja miongoni mwa wanaoshiriki. Michezo mingi kama vile mpira wa miguu au wa mikono, huhitaji ushirikiano ili kikundi kiweze kushinda, rede hukuza umoja miongoni mwa watoto.

Michezo huburudisha wanaoshiriki na vilevile wasioshiriki. Kwa mfano mchezo wa rede huburudisha watoto wanashiriki hasa wakiwa wametoka shuleni kwani huwaondolea uchovu. Mchezo wa mpira wa miguu huwaburudisha watazamaji; mfano mechi kati ya Simba Sports Club na Yanga huwaburudisha watazamaji.

Michezo ni njia mojawapo wa ajira kwa watu. Watu wanaoshiriki kwenye michezo kama vile michezo ya mpira wa miguu na wakikapu hulipwa kila mwezi na kila wanapocheza uwanjani. Tuchukulie mfano Bwana Samata wa Simba Sports club au Mcheza maarufu huko Marekani Stephen Curry wa Washington Warriors. Hawa hucheza (kushiriki kwenye michezo) na hulipwa.

Kwa ujumla watu wanaoshiriki kwenye michezo hupata faida. Ushauri wangu kwa watu ni wapende kushiriki kwenye michezo na wanaoshiriki waweze kupumzika mara kwa mara kama wale wanaokimbia; ili kutokuchiwa na hewa na kumfanya azimie au afe kabisa.

Kielelezo Na. 10.1: *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.*

Katika kielelezo Na. 10.1, mwanafunzi aliandika insha ya hoja kuhusu umuhimu wa michezo kwa kuzingatia taratibu zote za uandishi kama vile kichwa cha insha, utangulizi mzuri na katika kiini, alitoa hoja nne na ufafanuzi wenye mifano kwa kila hoja, hivyo kupata alama zote 15.

Hata hivyo, wanafunzi 286,831 sawa na asilimia 45.18 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kuandika insha zisizojitosheleza kwani hazikuzingatia vigezo vyote muhimu. Mapungufu yaliyobainika ni pamoja na kutoandika kichwa cha insha, utangulizi na kutoa maana ya neno *michezo* isiyo sahihi, kuandika sentensi ndefu zisizo na mkato wala kituo, na kutoa hitimisho lisiloendana na hoja walizozitoa katika kiini cha insha.

Licha ya ufaulu mzuri na wa wastani wa wanafunzi katika swali hili, baadhi ya wanafunzi (155,175) sawa na asilimia 24.44 walipata alama hafifu kutokana na kukosa maarifa na uelewa kuhusu uandishi wa insha za hoja. Baadhi yao, asilimia 3.8 walipata 0 kwa kuwa waliandika insha isiyozingatia vigezo stahiki, kama vile: kichwa cha insha kinachotakiwa kuandikwa kwa herufi kubwa; utangulizi wa insha wenye kueleza maana na aina ya michezo, kiini cha insha na hitimisho linaloendana na insha. Wapo wanafunzi walioshindwa kuandika insha kwa kuzingatia hoja walizopewa kuhusu *Umuhimu wa Michezo*, badala yake waliandika insha zinazohusu mambo mengine kama vile SHULE YETU, NCHI YETU; barua za kikazi na za kirafiki kuhusu umuhimu wa michezo; na wengine walinakili kifungu cha habari kilichopo katika swali la 3 la ufahamu kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika barua badala ya insha, hivyo kupata 0.



SHURE YA SECONDARI
S.L.P
SHINYANGA
1/11/2022

SHULE YA SECONDAR
S.L.P
KAHAMA
1/11/2022

YAH: UMUHIMU WA MICHEZO-
Husika na kichwa cha habari hapo juu kuwa
kwamba umuhimu wa michezo cha kwanza
umuhimu wa michezo ni kuuboresha mwili
kuimarisha mwili na kuchangamsha mwili
na vitu mbalimbali vina vyo uhusika na Michezo
Umuhimu wa kenye mchezo cha kwanza kwenye
mchezo (i) kumbia maana nyingine kupasha-

Kielelezo Na. 10.2: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.*

Katika kielelezo Na. 10.2, mwanafunzi aliandika barua ya kikazi kuhusu umuhimu wa michezo badala ya kuandika insha yenye hoja nne kuhusu *Umuhimu wa Michezo*. Licha ya mwanafunzi huyo kujibu kinyume na matakwa ya swali, bado alikuwa na makosa ya kitahajia kwa kuandika *SECONDAR* badala ya SEKONDARI na *kenye* badala ya kwenye, jambo linaloonesha kuwa mwanafunzi huyo hakuwa na umahiri wa kuandika Kiswahili sanifu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika mada tano (5) zilizopimwa katika somo la Kiswahili unaonesha kuwa mada nne zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada ya *Ufahamu* ilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu wa asilimia 91.55 ikifuatiwa na mada ya *Sarufi* (78.71%), *Uandishi wa Insha/Utungaji* (75.56%) *na* mada ya *Fasihi kwa Ujumla* (72.47%). Aidha, mada ya *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* ilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu cha asilimia 51.52. Takwimu zinaonesha kuwa katika upimaji huu, mada ya *Fasihi kwa Ujumla* ndiyo mada pekee iliyopanda kutoka kiwango cha wastani (55.85%) mwaka 2021 hadi kiwango kizuri (72.47%) kwa mwaka 2022. Mada nyingine nne zilipungua ufaulu kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka 2021.

Mada nne zilizokuwa na upungufu wa ufaulu kwa mwaka 2022 zikilinganishwa na mwaka 2021 ni *Ufahamu* kutoka asilimia 97.43 hadi 91.55, *Uandishi wa Insha/Utungaji* kutoka asilimia 86.29 hadi 75.56, *Sarufi* kutoka asilimia 79.42 hadi 78.71 na *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* kutoka asilimia 79.31 hadi 51.52 ambapo upungufu huo ulikuwa asilimia 5.88, 10.73, 0.71 na 27.79 mtawalia. Hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi ni wa wastani kwani kumekuwa na upungufu mkubwa wa viwango vya ufaulu katika mada nyingi ikilinganishwa na mwaka 2021.

Wastani wa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mada zote kwa mwaka 2022 ni asilimia 73.97, kiwango ambacho ni cha chini kwa asilimia 5.69 kikilinganishwa na mwaka 2021, ambapo wastani wa kiwango cha ufaulu kwa mada kilikuwa 79.66. Upungufu huu wa ufaulu kwa mwaka 2022 unathibitisha kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maswali yaliyopimwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2022, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi katika maswali mengi.

Hata hivyo, mada iliyokuwa na wastani wa chini wa ufaulu kwa mwaka 2022 ni mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha (*51.52%) iliyopungua kwa kiasi kikubwa zaidi cha asilimia 27.9, hali inayoashiria kuwa mada hii inahitaji kupewa kipaumbele zaidi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wake. Hii inatokana na wanafunzi wengi kukosa maarifa na ujuzi wa kutosha katika kufafanua sifa za misimu katika lugha ya Kiswahili na kueleza dhima za lugha

katika jamii. Kwa ujumla, mada hii inatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa na kuwafanya kuwa mahiri katika matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Ufaulu wa wanafunzi katika mada mbalimbali kwa mwaka 2022 umeainishwa katika **Kiambatisho A**. Pia, ulinganifu wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika mada kwa mwaka 2021 na 2022 umeainishwa katika **Kiambatisho B.**

## 4.0 HITIMISHO

Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2022 katika somo la Kiswahili ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia majazi ya utambuzi ambayo ni *kuelewa, kukumbuka, kutumia, kuchambua*, *kutathmini* na *kuunda*. Ufaulu wa wanafunzi kwa ujumla ulikuwa mzuri kwani asilimia 95.66 walifalu.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika upimaji huu kama vile; baadhi ya wanafunzi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizopimwa hususani mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha*. Aidha, wapo wanafunzi walioonesha kutokuzingatia matakwa ya maswali ipasavyo, hivyo kuwa na ufaulu hafifu au usioridhisha. Ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili, changamoto hizo zinaweza kutatuliwa kwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya kutosha na ya mara kwa mara kuhusu matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali, kuweka msisitizo katika matumizi ya kauli sahihi za kifasihi kama vile *methali, nahau, misemo na vitendawili* ili kuondokana na kuchanganya matumizi ya dhana za hizo. Vilevile, wanafunzi wapatiwe mazoezi ya kutosha katika mada za *Sarufi*, *Ufahamu* na *Uandishi* ili kuwajengea weledi katika mada hizo na kuimarisha ufaulu katika mada zote.

Kwa upande mwingine, uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika maswali yaliyopimwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa zipo jitihada kubwa zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali wa elimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2022 umeongezeka. Aidha, mada za *Ufahamu* na *Utungaji/Uandishi* zimeendelea kuwa na ufaulu wa kiwango kizuri cha zaidi ya asilimia 75 kwa miaka miwili mfululizo ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa 97.43% na 86.29% kwa mwaka 2021; 91.55% na 75.56% kwa mwaka 2022 mtawalia. Hata hivyo, mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* pekee ndiyo iliyokuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani kwa mwaka

2022. Kwa jumla, ufundishaji wa mada hii unahitaji kupewa kipaumbele zaidi ili kufikia kiwango kizuri cha ufaulu kwa miaka inayofuata.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi wa Kidato cha Pili inatarajiwa itumike ipasavyo ili kuwa chachu na dira ya mabadiliko kutoka viwango vya chini vya ufaulu kwenda viwango vya juu vya ufaulu katika mada mbalimbali. Aidha, taarifa hii itawawezesha walimu, wanafunzi na wadau wengine kuelewa changamoto mbalimbali zinazowakabili kwenye ufundishaji na ujifunzaji na kuzitatua ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa upimaji mwingine.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili, hususani katika mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* iliyokuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani, walimu wanashauriwa:

(a) kutoa mifano kadhaa ya misimu na kuwataka wanafunzi kueleza chanzo, sababu na matumizi ya misimu hiyo.

(b) kuongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazi mradi ya kukusanya na kujadili misimu inayotumika katika miktadha mbalimbali.

(c) kutumia mbinu ya igizo-dhima ili kuwaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa ili kuweza kutofautisha aina na sifa za misimu katika lugha ya Kiswahili.

(d) kutumia njia ya majadiliano na vielelezo vya kufundishia (zana za kufundishia) zinazopatikana katika mazingira halisi. Aidha, mada zote zifundishwe kwa vitendo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi kwa kulinganisha kinachofundishwa na uhalisia wake.

**KIAMBATISHO A:** UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2022

| **Na.** | **Mada** | **Ufaulu kwa kila Swali** | | **Wastani** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Na. ya Swali** | **% ya ufaulu (alama 30⁺)** | | |
| 1. | *Ufahamu* | 1 | 91.55 | 91.55 | Vizuri |
| 2. | *Sarufi* | 4 | 63.56 | 78.71 | Vizuri |
| | | 5 | 93.85 | | |
| 3. | *Uandishi wa Insha/Utungaji* | 10 | 75.56 | 75.56 | Vizuri |
| 4. | *Fasihi kwa Ujumla.* | 8 | 66.60 | 72.47 | Vizuri |
| | | 9 | 78.34 | | |
| 5. | *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* | 6 | 59.07 | 51.52 | Wastani |
| | | 7 | 43.97 | | |

**KIAMBATISHO B:** ULINGANIFU WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2021 NA 2022

